



TAARIFA KWA UMMA

KUONGEZA MUDA WA UDAHILI WA SHAHADA YA KWANZA KATIKA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NCHINI KWA PROGRAMU AMBAZO BADO ZINA NAFASI KWA MWAKA WA MASOMO 2021/2022

Dar es Salaam, Tarehe 11 Oktoba, 2021

1.0 UTANGULIZI

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) inapenda kufahamisha umma na wadau wa Elimu ya Juu nchini kuwa udahili katika awamu zote tatu kwa ngazi ya Shahada ya Kwanza katika Taasisi za Elimu ya Juu nchini kwa mwaka wa masomo 2021/2022 umekamilika kwa mujibu wa ratiba ya udahili iliyoidhinishwa na Tume.

2.0 KUFUNGULIWA KWA AWAMU YA NNE YA UDAHILI

Baada ya kukamilika kwa awamu zote tatu za udahili, Tume imepokea maombi ya kuongeza muda wa udahili kutoka kwa baadhi ya waombaji waliokosa udahili kutokana na sababu mbalimbali. Pia, Tume imepokea maombi ya kuongeza muda wa udahili kutoka kwa baadhi ya Taasisi za Elimu ya Juu nchini ambazo bado zina nafasi katika baadhi ya programu za masomo kwa mwaka 2021/2022.

Ili kutoa fursa kwa waombaji ambao hawakuweza kudahiliwa au hawakuweza kuomba udahili katika awamu tatu zilizopita kutokana na sababu mbalimbali, ***Tume imeongeza muda wa udahili kwa kufungua Awamu ya Nne na ya mwisho ya udahili inayoanza leo tarehe 11 Oktoba hadi 15 Oktoba, 2021.*** Tume inawaasa waombaji wote ambao bado hawajadahiliwa, watumie fursa hii vizuri ili kupata nafasi ya udahili.

3.0 UTARATIBU WA UDAHILI KATIKA AWAMU YA NNE

Tume inaelekeza waombaji wa udahili na vyuo kuzingatia utaratibu wa udahili katika Awamu ya Nne kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 1.**

Jedwali Na. 1 Utaratibu wa udahili katika Awamu ya Nne kwa mwaka wa masomo 2021/2022

Na.	Muda	Tukio
1.	11 - 15 Oktoba, 2021	Kutuma maombi ya udahili katika Awamu ya Nne.
2.	19 - 20 Oktoba, 2021	Vyuo kuwasilisha Tume majina ya waliodahiliwa katika Awamu ya Nne.
3.	24 Oktoba, 2021	Vyuo kutangaza majina ya waliodahiliwa katika Awamu ya Nne.
4.	3 - 24 Oktoba, 2021	Kuthibitisha udahili kwa wale walioshindwa kuthibitisha udahili wao katika awamu za udahili zilizopita kutokana na sababu mbalimbali.

4.0 WITO KWA TAASISI ZA ELIMU YA JUU NCHINI

Tume inatoa wito kwa Taasisi za Elimu ya Juu nchini zilizoidhinishwa kudahili kwa mwaka wa masomo 2021/2022, kutangaza programu zenye nafasi ili kuwawezesha waombaji kufanya maamuzi sahihi wakati wa kutuma maombi ya udahili na kuepusha usumbufu kwa waombaji kuomba programu ambazo hazina nafasi. Aidha, ***Tume inasisitiza Taasisi zote za Elimu ya Juu nchini kuzingatia idadi ya wanafunzi iliyoidhinishwa katika programu husika.***

Imetolewa na:


Prof. Charles D. Kihampa
KATIBU MTENDAJI
TUME YA VYUO VIKUU TANZANIA